THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1

ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2 **Jumatano, 17 Oktoba 2012 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote.**
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

MPENDAE SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 4714
LIBRARY
PLEASE MAINTAIN OUR BOOK

Scanned by CamScanner

SEHEMU A (Alama 10)
SUNNAH NA HADITH

1. Chagua jibu sahihi katika maswali (i) – (x) kisha uandike herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) "Na tumekuteremshia mawaidha ili uwabainishie yaliyoteremshwa kwao..." (16:44). Kutokana na aya ya hapo juu, Mtume (s. a. w) alitekeleza maagizo ya Mwenyezi Mungu kwa njia ipi?
A Alifanya kazi ya kuwafasiria masahaba wake aya moja ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu.
B Aliwabainishia baina ya halali na haramu katika yaliyoteremshwa ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu.
C Alikuwa hafundishi masahaba wake mawaidha anayoteremshiwa ila baada ya kuwabainishia na kuwawekea wazi aya zilizoteremshwa kabla.
D Aliweka wazi baadhi ya sharia na aya za Qur'an ambazo hazieleweki.
E Aliandika kwa mkono wake Qur'an yote tangu mwanzo hadi mwisho.

(ii) Kazi kuu ya Sunnah ya Mtume (s.a.w) imeelezwa katika aya ipi kati ya zifuatazo?
A "Mola wetu! Tumeyaamini uliyoyateremsha, na tumemfuata Mtume, basi Tuandike pamoja na washuhudiao"(3:53)
B Basi simamisheni Sala na toeni Zaka na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote. (58:13)
C Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho (59:7)
D Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu (47:33)
E Na Tumekuteremshia mawaidha ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao, na ili wapate kufikiri (16:44).

(iii) "Sunnatullah" kama ilivyotumika katika Qur'an ina maana ya
A mwenendo au mila aliyoelekezwa Mtume
B kawaida au desturi aliyoielekeza Allah
C desturi au kawaida ya Mtume
D mwenendo wa utekelezaji wa Uislamu
E tabia na mwenendo wa Allah.

(iv) Maudhui ni aina ya Hadith ambayo
A ni ya uongo aliyozuliwa Mtume (s.a.w) na hupingana na Qur'an
B wapokezi wake wote wana sifa ya kudhibiti maneno vizuri kama walivyoyapokea
C wapokezi wake wote ni watu wenye msimamo mzuri katika Uislamu
D Sanadi yake imeshikamana kuanzia mwanzo mpaka mwisho
E wapokezi wake ni waadilifu licha ya kuwa na upungufu wa kuhifadhi.

MPENDAE SECONDARY SCHOOLS
MAINTAIN OUR BOOK
P. O. Box 4714
LIBRARY

Scanned by CamScanner

(v) Bi Aisha mke wa Mtume alipoulizwa juu ya tabia ya Mtume alijibu: *"Tabia yake ilikuwa ni Qur'an."* Kauli hii ina maana kuwa
A hakuna tofauti baina ya Sunnah na Qur'an
B Mtume ndiye Mfasiri wa Qur'an
C Mtume alikuwa akisoma Qur'an kila wakati
D Mtume alikuwa akiishi kwa mujibu wa Qur'an
E huwezi kufuata Qur'an bila ya Sunnah ya Mtume.

(vi) Wachunguzi wa Hadith wamezikataa hadith zote zinazomkatalia msamaha wa Mwenyezi Mungu mtu aliyefanya madhambi makubwa katika maisha yake kutokana na
A Mapokezi yake
B Sanad yake
C Matini yake
D Udhaifu wake
E Kufichwa kwake.

(vii) Hadith za Sunnah zinazolingana na hadhi ya Qur-an ni
A Qudus
B Mutawatir
C Sahih Bukhar na Muslim
D Nabawiy
E Sahihi Muslim.

(viii) Kasema Mjumbe wa Allah: "Mtu anayechukua kamba na shoka lake, akaenda mwituni kutafuta kuni akabeba kichwani au mgongoni mwake akaziuza na pesa akazitumia kwa kununua chakula ni bora kuliko yule ambaye anaombaomba…. (**Bukar na Muslim**). Hadithi hii inatufundisha kuwa
A kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kujitegemea ni wajibu wa Waislamu
B ni Sunnah kutumia pesa uliyoifanyia kazi kwa kununulia chakula
C kufanya kazi za mikono kumehimizwa sana na Mtume
D Mtume anachukia sana watu wavivu na ombaomba
E kufanya kazi ili kujitegemea ni miongoni mwa Sunnah za Mtume.

(ix) Katika kipindi cha Masahaba miongoni mwa matatizo yaliyotatuliwa kwa kutumia hadith za mtume (s. a. w) ni
A pale waarabu katika mikoa mingi walipokataa kutoa Zakat.
B bibi Fatma (as) alipodai mirathi ya baba yake.
C zilipojitokeza tofauti za usomaji wa Qur'an kati ya masahaba.
D mzozo wa kuandama kwa mwezi baina ya nchi na nchi.
E kutafuta mwelekeo wa Kibla.

(x) Kigezo kilichotumika kuhakiki historia ya wapokezi wa hadithi ni
A ukweli na ucha Mungu wao
B kusilimu kwao
C umri na elimu yao
D kushiriki kwao Jihad
E utiifu kwa Mtume.

MPENDAE SECONDARY SCHOOL
HELP MAINTAIN OUR BOOK
P. O. Box 4714
LIBRARY

Scanned by CamScanner

SEHEMU B (Alama 15)
QUR'AN

2. Chagua kifungu cha maneno kutoka **orodha B** kinachowiana na kifungu cha maneno kutoka **orodha A**. Andika herufi ya jibu sahihi pembeni ya namba kutoka orodha A.

Orodha A		orodha B
(i)	Hakika sisi ndiyo tulioteremsha mawaidha haya (hii Qur'an) na hakika sisi ndiyo tutakaoyalinda (15:9).	A. Njia anazotumia Mwenyezi Mungu kuwasiliana na waja wake.
(ii)	Hebu mwanadamu atazame chakula chake (80:24).	B. Uthibitisho kuwa Qur'an ni maneno ya Mwenyezi Mungu.
(iii)	"Ee mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. Basi fikiri, waonaje?" (37:102).	C. Mtume Muhammad (s.a.w) ni kiigizo cha Waislamu.
(iv)	.....Basi muamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, aliye Nabii Ummy ambaye humuamini Mwenyezi Mungu na maneno Yake. Na mfuateni yeye mpate kuongoka (7:158).	D. Qur'an haitaingiliwa na mkono wa binadamu.
(v)	... Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine. ... (39:7).	E. Mwenyezi Mungu hakutuamrisha kusoma elimu za Fiqhi pekee.
(vi)	"Enyi wanadamu ! Shetani (ibilisi) asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika pepo..."(7:27).	F. Malaika Jibril (a.s).
(vii)	Uteremsho wa kitabu hiki hauna shaka kuwa umetoka kwa Mola wa walimwengu (32:2).	G. Wanadamu hawana budi kuongozwa na Qur'an.
(viii)	... Kwa hakika wanaomuogopa mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wale wataalamu....(35 : 28).	H. Qur'an si maneno ya Mtume (s.a.w).
(ix)	Tutakusomesha (Tutakusomea) wala hutasahau. Ila akipenda Mwenyezi Mungu; Yeye anajua yaliyo dhahiri na yaliyofichikana (87:6-7).	I. Dalili za kuwepo Allah (s.w) zipo katika kila kitu.
(x)	....na kitabu tulichokuletea kwa wahyi ndicho cha haki; kinasadikisha (vitabu) vilivyokuwa kabla yake(35:31).	J. Majina ya Qur'an.
(xi)	Watakaojitenga nayo, basi kwa yakini watabeba siku ya kiama mizigo (ya dhambi) (20:100).	K. Kuwa mnyenyekevu wakati wa kusoma Qur'an.
(xii)	Suratut Alaq (96:1- 5).	L. Wahy ni ujumbe anaopata mwanadamu kutoka kwa Allah (s.w).
(xiii)	Ni amani (usiku) huo mpaka mapambazuko ya alfajiri. (97:5).	M. Udhaifu wa madai ya Rushdie.
(xiv)	Kwa hakika hii (Qur'an) ni kauli (aliyokuja nayo) mjumbe mtukufu (81 :19).	N. Lailatul- qadri.
(xv)	... mfalme, mtakatifu, mwenye salama mtoaji wa amani, mwenye kuyaendesha mwenyewe mambo yake, mwenye shani... (59 :23).	O. Kushuka kwa Qur'an.
		P. Majina ya Allah.
		Q. Allah ni mjuzi mwenye hekima.
		R. Al Furqaan.
		S. Siku ya malipo.
		T. Jabal Hiraah.

Scanned by CamScanner

SEHEMU C (Alama 15)
TAWHIID

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Mwenyezi Mungu ametaja sifa zake tukufu katika Suratul A'laa (87:1-5) kama ifuatavyo:
- (i) Kisha Akaifanya mikavu yenye kupiga weusi.
- (ii) Na Akakikadiria (kila kimoja jambo lake) na Akakiongoza (kufanya jambo hilo)
- (iii) Litukuze Jina la Mola wako aliye Mtukufu
- (iv) Na aliyeotesha ndisha (malisho)
- (v) Aliyeumba (kila kitu na) akakitengeneza

(b) Mtazamo wa Uislamu juu ya maana ya dini unaelezeka kama ifuatavyo:
- (i) Uislamu ndiyo dini pekee inayomletea mwanadamu faraja na furaha kwa sababu imetumwa na Allah (sw) aliye mjuzi na mwenye hekima.
- (ii) Dini isiyokuwa ya Allah (sw) humuelekeza mwanadamu kwenye maisha ya upotevu yenye dhiki na dhuluma.
- (iii) Hivyo, tafsiri ya makafiri kuwa dini ni imani juu ya Mungu muumba si tafsiri sahihi.
- (iv) Dini ziko nyingi lakini Uislamu ndiyo dini pekee anayoiridhia Allah (sw) kama Qur' an inavyosisitiza: "Bila shaka dini mbele ya Allah ni Uislamu." (3:9).
- (v) Dini ni mfumo wa maisha anaoufuata mwanadamu katika kuendesha maisha yake ya kila siku ya kibinafsi na ya kijamii.

(c) Suratut Tyn kama ilivyotafsiriwa katika Qur'an.
- (i) Je! Allah si hakimu muadilifu kuliko mahakimu wote?
- (ii) Basi ni lipi likupalo kukadhibisha malipo baada (ya kuona hayo)?
- (iii) Bila ya shaka tumemuumba mwanadamu kwa umbo lililo bora kabisa. Kisha tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini.
- (iv) Ila wale wenye kuamini na kutenda mema, watakuwa na ujira usiokwisha, (unaoendelea maisha).
- (v) Naapa kwa Tini na Zaituni. Na kwa mlima Sinai. Na kwa mji huu (wa Makka) wenye amani.



Scanned by CamScanner

SEHEMU D (Alama 30)
FIQH

4. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi kwa kuandika majibu yako katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) (i) Nini maana ya Fiqh?
(ii) Taja matapo mawili ya Fiqh.
(b) Elezea kwa kifupi nguzo mbili za swala zinazotekelezwa kwa kusomwa katika kisimamo na kabla ya kutoa salamu.
(c) Fafanua mambo mawili tu ambayo humfanya Muislamu kutofikia lengo la swala.
(d) Elezea tofauti iliyopo kati ya kiasi cha zakat kwa mkulima aliyeotesha mazao yake kwa mvua za msimu na mfugaji wa ng'ombe.
(e) Elezea tofauti iliyopo kati ya muda unaostahiki kutoa zakat ya mazao ya shambani na muda unaostahiki kutoa zakat ya mali ya Biashara.
(f) Elezea maana ya swaumu na lengo lake katika Uislamu.
(g) Zakatul-fitr ni nini? Taja makundi mawili ya watu wanaostahiki kupewa Zakatul-fitri.
(h) Orodhesha ibada mbili za Hija ambazo Haji anatembea au kuzunguka na kisha toa maelezo ya ibada hizo kwa ufupi.
(i) Ibada ya Hija hufanyika katika maeneo manne maalum (matakatifu). Taja maeneo hayo.
(j) Taja vikwazo viwili vya ndoa kwa mume muoaji.
(k) Kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu mke aliyepewa talaka hutakiwa kufanya nini kabla ya kuamua kuolewa tena?
(l) (i) Elezea maana ya haki katika Uislamu.
(ii) Orodhesha aina mbili za haki zilizofungamana na mali ya urithi zilizotajwa katika Qur'an.
(m) Taja aina nne za vipawa alivyotunukiwa mwanadamu vinavyomtofautisha na mnyama.
(n) Ainisha njia mbili ambazo zitasababisha uchumi wa Kiislamu kuhesabika kuwa ni haramu kwa mujibu wa sheria.
(o) Shahada ndio kiingilio cha Uislamu kutoka kwenye dini nyingine yeyote; hivyo shahada ya kweli ni lazima idhihirike katika sehemu tatu. Elezea kwa kifupi sehemu mbili.



Scanned by CamScanner

SECONDARY SCHOOL
MAINTAIN OUR SOCIETY
P. O. Box 4714
LIBRARY

SEHEMU E (Alama 30)
TAREKH

5. Chagua **neno** au **kifungu cha maneno** (i) – (xxx) ili kukamilisha kauli (a) – (o) kwa usahihi. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

(i)	Mussa (a.s)	(xi)	Harun (a.s)	(xxi)	Ubabe na ukandamizaji
(ii)	Makka	(xii)	Lut (a.s)	(xxii)	Yusufu (a.s)
(iii)	Hud (a.s)	(xiii)	Saleh (a.s)	(xxiii)	Ibrahim (a.s)
(iv)	Kutubu	(xiv)	Waddi	(xxiv)	Gharika
(v)	Makafiri	(xv)	Allah (s.w)	(xxv)	Mtu
(vi)	Firauni	(xvi)	Ufasaha	(xxvi)	Shirk
(vii)	Ismaili (a.s)	(xvii)	Sodoma na Gomora	(xxvii)	Nduguze
(viii)	Ad	(xviii)	Miungu ya masanamu	(xxviii)	Muhammad (s.a.w)
(ix)	Wanadamu	(xix)	Suwaa	(xxix)	Safina
(x)	Lengo	(xx)	Adam (a.s)	(xxx)	Mtume

Maswali

(a) Dhana ya _____ ni kuwa ulimwengu na vyote vilivyomo vimezuka tu na hakuna _____ maalumu la kuwepo kwake.

(b) Kwa mujibu wa Qur'an asili ya maumbile yote ulimwenguni ni _____ na yametiishwa kwa _____ ili waweze kufikia lengo la kuumbwa kwao.

(c) Nabii Adamu (a.s) ni _____ na _____ wa kwanza hapa duniani.

(d) Ibilisi alikataa kutiii amri ya Allah (s.w) ya kumsujudia Adam (a.s) badala ya _____ kwa Mola wake kwa makosa aliyoyafanya alichukua kisasi dhidi ya _____ na kizazi chake kwa kuwafanya wapotee.

(e) _____ sanamu la sura ya kiume na _____ sanamu la sura ya kike ni miongoni mwa miungu ambayo iliabudiwa na watu wa Nabii Nuhu (a.s).

(f) Waliokataa ujumbe wa Nabii Nuhu (a.s) waliangamizwa kwa _____ na waumini wachache waliokolewa kwa _____.

(g) Nabii _____ alitumwa kwa watu wa _____ waliokuwa maarufu kwa teknolojia ya kujenga majumba marefu.

(h) Makafiri walimwambia Nabii _____ na walioamini pamoja naye kuwa wameleta nuksi katika nchi kwa kuikataa _____.

(i) Nabii _____ na _____ walitokea kupigwa mawe na watu wao katika harakati zao za kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu.

(j) Mji wa _____ katika nchi ya Hijaz alipokuwa akiishi _____ ulifanywa kuwa makao makuu ya harakati za kuhuisha Uislamu wakati wa Nabii Ibrahim (a.s.).

(k) Nabii _____ alitumwa kulingania Uislamu katika mji wa _____.

(l) Tabia njema ya Nabii _____ ilimfanya apendwe zaidi na baba yake kuliko _____.

(m) Nabii _____ alitumwa kuwakomboa Bani Israil kutokana na dhuluma waliyokuwa wanafanyiwa na _____.

(n) Mussa (a.s) alimuomba Allah (s.w) amfanye ndugu yake _____awe msaidizi wake katika kazi ya Da'awa kwa _____ wake wa kuongea.

(o) Wakati anazaliwa Mtume Muhammad (s.a.w) karne ya 6 _____ yalifanywa matendo ya kishujaa na ya kujivunia wakati _____ iliota mizizi kiasi cha watu kutembea na miungu mfukoni.

Scanned by CamScanner